**Learning by Ear – ELIMU NA KAZI**

**Elimu ya chuo kikuu - Hadithi ya Malaika / Episode 06**

**Mwandishi: Njoki C. Muhoho**

**Mhariri: Maja Dreyer**

**Tafsiri: Eric Ponda**

WAHUSIKA:

Mtangazaji - Mwanaume

Malaika - Msichana miaka 23

Daniel - Mvulana miaka 24

Ms Grace - Miaka 52 . Mwalimu na mnasihi wa Malaika.

Auntie Tizo - Miaka 64. Shangaziye Malaika.

Elder Nathan - Miaka 60 Babake Malaika.

Mama Rose - Miaka 45 mamake Malaika.

**INTRO**

**MUZIKI**

**1. MTANGAZAJI** Hujambo na karibu kwa makala yetu ya sita na ya mwisho katika mfululizo huu wa vipindi vya “Learning by Ear” `Noa bongo jenga maisha yako´, tukizungumzia hadithi ya Malaika na jinsi anavyomudu masomo na maisha ya chuo kikuu. Katika kipindi kilichotangulia, tulisikia jinsi rafiki yake Daniel alivyomsaidia kutafutia shirika alikofanyia

mazoezi ya mafunzo kuhusu utendaji kazi, hadi kumaliza na kufanya mtihani wake wa mwisho.Sasa familia yake ndio mwanzo imerejea kijijini kutoka sherehe hizo za kufuzu kwa binti yao jijini, na bado sherehe hizo zinaendelea Kijijini humo.

**SCENE 1:NYUMBANI KWA MZEE NATHAN**

**SFX:** ***SAUTI ZA NGOMBE NA MBUZI WAKILIA, WATU WAKIPIGA GUMZO NA KUSHANGILIA KWA MBALI***

2. MZEE NATHAN …na kisha …huyu mwanamke aliyevalia mavazi ya ajabu na unyoya…

3. MALAIKA *(**akimkatiza**)* Muhadhiri mkuu, Baba, Muhadhiri mkuu!.

4. MZEE NATHAN ...sawa, huyo mhadhiri mkuu, alisema "..kwa mamlaka niliyotunukiwa na baraza kuu la chuo hiki, nawatuza wanafunzi hawa shahada ya digrii ya kwanza ya masuala ya sayansi baada ya kutahiniwa na kupita mitihani yao. ….Malaika Kamau...!

**5. WOTE Nderemo, vifijo na vigelelegele**

6. MAMA ROSE : Tunafurahia na kujivunia ufanisi wako binti yangu!

7. MZEE NATHAN : Ana akili kama yangu.

8. SHANGAZI TIZO : Kakangu, mbona unasahau haraka hivi …? kwamba ulitaka kumuoza binti yetu…eti ana akili kama yangu …hata huna haya kopeni kaka!.

9. MALAIKA : Baba, shangazi Tito, tosha! nyote mlinisaidia kufika nilipo sasa, na najua jinsi nitakavyo mlipa kutokana na juhudi zenu. Mnajua bado hatujalipa ule mkopo.

10. SHANGAZI TIZOSi wewe uliyechukua mkopo huo, ni sisi! Kama tu vile tulivyo kuja pamoja kutafuta pesa hizo, pia tutakutana tena kutafuta njia za kulipa mkopo huo.

**SFX:** ***NYAYO ZIKIKARIBIA***

11. MWALIMU GRACE Malaika.. Malaika… Nina barua yako..

12. SHANGAZI TIZO Mwalimu Grace, ni nini? Ni nini? Au mkopo tuliochukua?

**SFX:** ***BARUA YAFUNGULIWA,MCHAKARISHO WA KARATASI***

13. MALAIKA … inatoka idara ya wafanyakazi serikalini.

**SFX: KARATASI ZIKIFURUKUTWA FURUKUTWA**

14. MALAIKA Inasema, “Tunafuraha kukujulisha kwamba umeajiriwa kama afisa wa kilimo nyanjani. Eneo lako la kuhudumu ni wilayani Kiambu…

15. WANAWAKE WOTE: *(Shangwe na nderemo)* Aliiliiiliiii

16. SAHANGAZI TIZO: Ullilililili……. Nimefurahi sana binti yangu, umepata kazi!!

17. MALAIKA : Hata mimi nimefurahi kupata kazi karibu na nyumbani….

18. SHANGAZI TIZO: Na ilikuwaje mpaka kukuajiri na kisha kukutuma ufanye kazi hapa nyumbani?

19. MWALIMU GRACE Shangazi Tizo, ungekuwa umeenda shule, ungejifunza mambo haya. Kabla ya kumaliza masomo mtu hutuma maombi katika ofisi za mashirika mengi tu. Na pia unaweza kutuma maombi ya kutafuta kazi serikalini kupitia idara ya usimamizi wa wafanyakazi. Lakini pia unaweza kufanya kazi kwa mashirika au kampuni za kibinafsi.

20. MZEENATHAN : Malaika! hebu njoo hapa,miaka mine iliyopita uliniambia kwamba unataka kuboresha kilimo na kiwango cha utoaji maziwa. Kwa hilo umefaulu, lakini bado nakukumbusha, nataka

uanze kutafuta mchumba, wewe si msichana mdogo tena..!

21.MTANGAZAJI Malaika sasa anasherehekea ufanisi wake na pia kupata kazi. Ufanisi huo sio wake binafsi bali kwa kijiji kizima. Lakini babake bado hajasaua kauli yake kwamba ni sharti apate mchumba na kuolewa. Baadaye siku hiyo…

**MUZIKI**

**SCENCE 2: NYUMBANI KWA MZEE NATHAN.**

**SFX: SAUTI ZA KIJIJINI NA CHENENE ZASIKIKA**

22. SHANGAZI TIZO : Kwa nini umekasirika, hii ni siku yako!

23. MALAIKA Shangazi umewaona wasichana wengine tuliokuwa pamoja? Sasa wameolewa na wamekuwa mama watoto. Na furahi kwa elimu niliyopata, lakini…

24. SHANGAZI TIZO Lakini nini tena? Wewe ni kielelezo hapa kijijini.

25. MALAIKA : Lakini mstakabala wangu ni upi? Ukizingatia tamaduni na kiwango cha kijijini, nafaa niwe nimeolewa na mama wa watoto wanne, na huku ndio mwanzo naanza maisha ya

taaluma. Sasa marafiki zangu watakuwa akina nani? Heh nani?

26. SHANGAZI TIZO Usijali.

**SFX: GARI INAKARIBIA: MLANGO UNAFUNGULIWA**

27. SHANGAZI TIZO Yule ni nani? Malaika, maafisa wa serikali wamekuja kukuchukua ukaanze kazi mara moja hii?

**28. WOTE WACHEKA**

**SFX:*NYAYO ZIKIKARIBIA*.**

29. MALAIKA : ***(anasisimkwa)*** Daniel! Daniel! umefika, nimefurahi kukuona!

30. SHANGAZI TIZO: Uuuiiii, je namuona msichana wetu akipepesa macho yake?

31. DANIEL : Habari za mchana nyote. Shikamoo!

32. WANAWAKE WOTE : Njema/ Marahaba

33. MZEE NATHAN : Kijana, wewe ni nani?

34. MAMA ROSE : Mume wangu mbona unakosa heshima?

35. MALAIKA : Anaitwa Daniel… baba huyu ni rafiki yangu tangu chuoni...

36. SHANGAZI TIZO Kweli, Mungu ni wa miujiza.

37. **MTANGAZAJI** :Malaika amepata mafanikio makubwa, lakini bado anajihisi upekwe kijijini. Je atamudu vipi tofauti ya maisha ya kijijini na hali aliyoko sasa kama mwanamke aliyesoma na pia matarajio ya wanakijiji?

**<u>SCENE 3: NYUMBANI KWA MZEE NATHAN.HALI YA UKIMYA</u>**

**SFX: NI USIKU : SAUTI ZA CHENENE, MOTO UKIWAKA.**

38. SHANGAZI TIZO: Kijana, serikali pia inakupa gari?

39. DANIEL : Sahamani, sikuelewi..

40. MALAIKA : Anadhani unafanya kazi serikalini.

41. DANIEL Ooh hapana, sifanyi kazi serikalini. Mimi nafanya kazi na kampuni ya kibinafsi

42. SHANGAZI TIZO : Sasa umetumwa na serikali?

43. MALAIKA : Auntie, ungefaa kuwa wakili wewe.

44 MWALIMU GRACE : Afisa wa polisi afadhali.

**45. WOTE WACHEKA**

46. DANIEL : Mimi nilituma maombi ya kutafuta kazi katika sekta ya kibinafsi, na kisha nikaajiriwa baada ya kuhojiwa na mameneja wa kampuni hiyo.

47. SHANGAZI TIZO: Yaonekana wanakulipa vizuri. Malaika, kwa nini usiajiriwe huko ili tuweze kulipa mkopo na uwe na gari pia wewe!

48. MALAIKA : Shangazi, wengine hutafuta kazi nje ya nchi, lakini mimi tayari nimefanya uamuzi nataka kufanya kazi na serikali nisaidie watu wangu. Napendelea kufanya kazi na serikali ili niwasaidie watu wangu. Nataka kufanya kazi hapa kijijini na wala sio mjinib au nchi ya kigeni. Kisha baadaye nitatafuta kazi kwingineko ambako itanilipa vizuri na kupata ujuzi zaidi.

49. MZEE NATHAN: Wewe ni msichana mwenye busara kama babako!

50. SHANGAZI TIZO Na kuhusu ule mkopo…siwezi kumsukuma Mungu anipe pesa. Ni lazima mtu ajitokeze kuleta pesa hizi.

51. MALAIKA : Nitatumia ujuzi niliopata kuboresha mazao ya kilimo. Tutapata mazao mazuri na pia ng’ombe hawa wataanza kutoa maziwa mengi. Pesa tutakazopata tutalipa mkopo kwa njia nafuu zaidi. Kadhalika nitaweza kuweka akiba ya mshahara wangu kulipa mkopo huo polepole.

52. MZEE NATHAN Wewe ni msichana mwenye busara sana, ni kama babako tu!

53. SHANGAZI TIZOKakangu sasa umeanza kunikera. Busara hiyo ilianza lini? Unakumbuka wewe ulitaka kumuoza msichana huyu mara ya kwanza.

54. MZEE NATHAN Tukizungumzia suala hilo la ndoa, unajua sasa binti yangu ana thamani gani ya ng'ombe?

55. MAMA ROSE : Nathan, tosha ….

56. DANIEL : Sikubaliani nawe, Mzee.…

57. MZEE NATHAN Nini? Unafikiri utaweza kumchukua binti yangu hivi hivi? hebu nikueleze... nyinyi vijana wa siku hizi...

58. SHANGAZI TIZO ***(amkatiza)*** Nyamaza Nathan...

59. MAMA ROSE Ooooiiii….

60. MALAIKA Baba!

61. DANIEL ***(anaendelea)*** Mzee nilitaka kusema… thamani yake sio idadi ya ng'ombe unaowafikiria, ni zaidi… na fahali… mkubwa kisha..!

**62. WOTE WACHEKA.**

OUTRO

63. **MTANGAZAJI** Ujasiri na uamuzi wa busara aliochukua Malaika kushinikiza kujiunga na elimu ya chuo kikuu, sasa umemzalia kuzaa matunda. Yale yaliyoonekana kuwa hayawezekani yamebainika kinyume. Ameweza kukabiliana na changamoto za maisha na tamaduni zinazowazuia wasichana kuendelea na elimu ya juu. Kwa kuzingatia maono yake na kufanya bidii masomoni licha ya mabadiliko ya mazingira,amepata na kukiletea sifa kijiji chake.Nyota yake inazidi kung´ara, kwani hivi sasa ana elimu, kazi na labda Mchumba. Hii ilikuwa makala ya sita na ya mwisho ya mfululizo wa vipindi vyetu vya 'Learning by Ear' kuhusu elimu na masiaha ya chuo kikuu. Mchezo huu umeandikwa na Njoki Muhoho. Ikipenda kusikiliza tena kipindi hiki na vingine, tembelea ukurasa wetu wa Mtandao www.dw-world.de/lbe. Hadi wakati mwengine Kwaheri.